JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

## UFAFANUZI KUHUSU USALAMA WA KINYWAJI CHA JUISI YA EMBE YA AZAM

**Dar es Salaam, 03 Februari, 2023**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kutoa ufafanuzi wa kitaalam juu ya taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu bidhaa ya juisi ya embe ya Azam inayozalishwa na kiwanda cha Bakhresa Food Products Limited kuwa na kiambato kiitwacho "*Sodium benzoate (E211)"* ambacho kimedaiwa kuwa si salama kwa afya ya watumiaji.

Tungependa kuondoa hofu kwa watumiaji wa bidhaa hiyo na kuufahamisha umma kuwa vitunzio (preservatives) vya *Sodium benzoate* hutumika katika kuhifadhi vyakula na vinywaji mbalimbali kwa kiasi kinachokubalika na vinaruhusiwa kwa mujibu wa kanuni za uzalishaji bora *(Good Manufacturing Practices)*, viwango vya kitaifa na kimataifa mfano FAO/WHO *Codex Alimentarius Commission (Codex General Standard for Food Additives),* ili kuzuia bidhaa zisiharibike na ziweze kukaa katika soko kwa muda uliokusudiwa.

Tafiti zilizokwishafanyika zinaonesha kuwa upo uwezekano wa *Sodium benzoate* kubadilika kikemikali na kuzalisha *Benzene* kutokana na uwepo wa *Ascorbic acid.* Kutokana na tafiti kuonesha kwamba kiasi cha kemikali hiyo kwenye vinywaji kiko chini ya kiwango kinachoweza kuleta madhara ya kiafya kwa mlaji, Shirika la Afya Duniani (WHO), Marekani na Umoja wa Ulaya hawajaweka matakwa ya kisheria *(legal requirements)* ya *Benzene* kwenye bidhaa hizi na kwamba udhibiti wa *Benzene* hufanyika kwa kutumia kiwango cha *Benzene* kwenye maji *(as reference)* ambacho hakitakiwi kuzidi 10 µg/kg (ppb).

TBS kupitia mifumo yake ya udhibiti ubora na usalama, imekuwa ikifanya ukaguzi kiwandani, uchunguzi wa kimaabara wa kiasi cha *Sodium benzoate* pamoja na vipimo vingine na ufuatiliaji wa bidhaa hiyo katika soko, ambapo kwa mwaka 2022 matokeo yamekuwa yakithibitisha kuwa bidhaa husika inakidhi vigezo vinavyokubalika kwa mujibu wa viwango. Aidha *Cellulose gum* au *Sodium carboxymethyl cellulose* (Sodium CMC) (E466) ambayo hutokana na mimea na sio mifupa au manyoya ya wanyama kama mtoa taarifa alivyoeleza hutumika katika bidhaa mbalimbali za chakula.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800 110 827.**

Imetolewa na:

**Gladness H. Kaseka**
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023